Mwongozo wa Misaada

DENVER
HOUSING STABILITY

Idara ya kuhakikisha udhabiti wa Makaazi (Housing Stabilty) husaidia kujenga Jumuiya ya Denver yenye afya njema, makaazi bora na iliyounganika. Idara hii huwekeza rasilimali, kuunda sera na kujenga mahusiano na mashirika ili kukuhifadhi katika nyumba yako, kusuluhisha hali ya ukosefu wa makaazi haraka,
na kukuunganisha na nafasi za kuwa na makaazi ya bei nafuu. Piga simu kwa 3-1-1 kwa taarifa zaidi au wasiliana kupitia denvergov.org/housing. **Para información en español visite denvergov.org/housing/**.

Je, Unastahiki kupata nafuu ya Ushuru au Kodi?

Mpango wa Denver wa **Utoaji nafuu ya Ushuru wa Mali** unarejesha sehemu ya kiasi cha ushuru wa mali uliolipwa, au kiwango sawa na kodi ya nyumba, kwa wakaazi wa Denver wanaostahiki.
Piga simu kwa nambari 720.944.4347 au denvergov.org/propertytaxrelief.

Jimbo la Colorado lina mpango wa **Kuahirisha Malipo ya Ushuru wa Mali** kwa watu wakongwe na kwa wanajeshi wanaohudumu, pamoja na kuwaondolea ushuru wakongwe, walemavu na wanajeshi waliostaafu.
Piga simu kwa nambari 720.913.9500 au wasiliana kupitia Colorado.gov/pacific/treasury/senior-and-veteran-property-tax-programs.

Je, Unahitaji msaada kulipa kodi au kulipa gharama za matumizi ili kuzuia Kufurushwa?

Mpango wa Kutoa **Msaada wa muda wa Kodi na matumizi** (TRUA) unaweza kutoa pesa za dharura kulipia kodi ya nyumba na kulipia gharama za matumizi kwa watu wanaostahiki. Piga simu kwa 3-1-1 na ubonyeze 6.

Huduma za Denver Human Services hutoa msaada wa kushughulikia **Kufurushwa na msaada wa kodi** kwa watu ambao wanakabiliwa na tisho la kupoteza makaazi yao na wanaostahiki kipato. Piga simu kwa nambari 720.944.4DHS (4347) au wasiliana kupitia kwa mtandao denvergov.org/humanservices.

Nafasi za Makaazi kwa waathiriwa wa UKIMWI (HOPWA). Msaada hutolewa Denver kupitia kwa Colorado Health Netwrok, ikijumuisha huduma za kodi, uraibu wa dawa za kulevya na afya ya Kiakili Piga simu kwa 303.837.0166 au kupitia kwa mtandao coloradoaidsproject.org.

Mpango wa Kulipia Umeme kwa Watu wa Kipato cha Chini (LEAP) ni mpango wa serikali kuu unaotoa msaada kwa wakaazi kulipia sehemu ya gharama za kupasha nyumba joto Msimu wa Baridi kali Piga simu kwa nambari 1.866.HEAT.HELP (1.886.432.8435) au wasiliana kupitia kwa mtandao denvergov.org/LEAP.

Msaada wa Kulipa gharama za Matumizi unaweza kutolewa kwa wale ambao hawawezi kulipa gharama za umeme za makaazi yao kupitia kwa Energy Otreach Colorado. Piga simu kwa nambari 1.866.HEAT.HELP (1.866.432.8435) au wasiliana kupitia kwa mtandao https://www.energyoutreach.org/programs-for-individuals/bill-payment-assistance/

Unahitaji kufanya marekebisho ya kurahisisha kufikia nyumbani kwako?

Kwa ushirikiano wa jiji na kupitia kwa halmashauri ya Denver Urban Renewal, mpango wa **Renter/ Homeowner Access Modification** huwasaidia wakaazi wenye ulemavu kufanya marekebisho yanayosaidia kufikia makaazi yao. Mkaazi au mwenye nyumba anaweza Kujaza. Piga simu kupitia nambari 303.534.3872 au kupitia renewdenver.org.

Je, unahitaji msaada kufanya ukarabati?

Jiji hushirikiana na Halmashauri ya Denver Urban renewal (DURA) kutoa mikopo yenye riba ya chini, kutoa misaada ya kufanya ukarabati wa dharura kwa makaazi, kufanya marekebisho ya kuimarisha na kurahisisha ufikiaji. Halmashauri ya DURA pia hutoa huduma za bila malipo za kuondoa hatari zinazotokana na madini ya risasi.

Wasiliana kupitia 303.534.3872 au renewdenver.org.

Unalenga kuepuka Kunadiwa?

Colorado Foreclosure Hotline hushirikiana na mashirika ya kutoa msaada wa ushauri kuhusu Makaazi.
Wasiliana kupitia 1.877.601.HOPE.

Huduma za ushauri kabla ya kununua na wakati wa kulipia makaazi kwa mpango wa rehani zinapatikana kutoka kwa Colorado Housing Assistance Corporation Wasiliana kupitia 303.572.9445 au kupitia chaconline.org.

Iwapo una hofu kuhusu mikopo isiyofaa au huduma za kifedha zinazoibua shinikizo, Ofisi ya Denver ya Uthabiti na Ulinzi wa Kifedha (Financial Empowerment and Protection) inaweza kukuelekeza kwa ushauri wa kifedha bila malipo kupitia kwa mpowered. Wasiliana kupitia 720.944.2498 au mtandaoni kupitia mpoweredcolorado.org.

Unahitaji ushauri wa Wapangaji au Mwenye nyumba au ushauri wa Kisheria?

Mwongozo wa Wenye nyumba na Wapangaji wa bila malipo wa Denver unapatikana kwa wapangaji wote ikiwemo vijana, watu wazima, wakongwe, watu waliohamia, wakimbizi, LGBTQ na watu wenye ulemavu. Zuru denvergov.org/housing.

Mpango wa Brother's Redevelopment unatoa ushauri kuhusu haki kwa wapangaji/wenye nyumba na hutoa rufaa. Huduma kupitia kwa simu zinapatikana kupitia 1.800.926.6623.

Denver ina miradi miwili inayotoa huduma za kisheria za gharama ya chini na za bila malipo. Wasiliana na Colorado Affordable Legal Services Kupitia kwa nambari 303.996.0010 au mtandaoni kupitia coloradoaffordablelegal.com. Wasiliana na Colorado Legal Services kwa simu 303.837.1313 au mtandaoni kupitia coloradolegalservices.org.

Je, Unataka Kupanga nyumba ya bei nafuu?

ColoradoHousingSearch.com ndio tovuti ambayo inatoa taarifa za kina na kuorodhesha makaazi ya kupanga ya bei nafuu katika Denver, eneo hili na katika Jimbo. Tovuti hii ina nyumba za watu binafsi pamoja na zile za idara ya Makaazi.

Vocha za Housing Choice (Sehemu ya 8) zinaweza kupatikana kupitia kwa halmashauri ya Makaazi ya Denver (DHA) kwa wale wanaostahiki Tafadhali wasiliana kupitia kwa 720.932.3000 au denverhousing.org.

Je, Unataka kununua Nyumba?

Ushauri wa bila malipo kwa wanaonunua makaazi unapatikana kupitia kwa mashirika yanayotoa misaada. Zuru denvergov.org/ housing au hud.gov.

Msaada wa kufanya malipo ya kwanza na kulipa malipo ya mwisho unapatikana kupitia mpango wa Denver wa metroDPA.. Piga simu kwa nambari 720.913.1534 au wasiliana kupitia mtandao denvergov.org/housing. Msaada wa kufanya malipo ya kwanza unapatikana kwa Colorado Housing Assistance Corp kupitia 303.572.9445 au chaconline.org.